



UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF ENERGY
ENERGY AND WATER UTILITIES
REGULATORY AUTHORITY
(EWURA)



PUBLIC NOTICE

SUSPENSION AND REVOCATION OF PETROLEUM PRODUCTS RETAIL LICENCES

Dodoma, 4th March 2026.

The Energy and Water Utilities Regulatory Authority (EWURA) hereby informs the public that it has revoked a Petroleum Retail Licence No. PRL-2018-269 issued to Iyan Energy Limited of Dar es Salaam to undertake petroleum retail business at Plot No. 26 & 27, Pangani Road, Tanga City in Tanga Region, and suspended for six months, Petroleum Retail Licence Number PRL-2022-296 issued to Crescent Energy Tanzania Limited to undertake petroleum retail business at Plot No.5, Block 'N', Chamakweza Area, Chalinze District Council in Pwani Region, both for violating the law and licence terms and conditions.

The decisions to revoke and suspend the licences were made after the Authority satisfied itself that Iyan Energy Limited and Crescent Energy Tanzania Limited have been engaging in selling or offering for sale petroleum products as wholesalers contrary to Section 131 of the Petroleum Act, Cap. 392 and Rule 9 and 11 of the Petroleum (Wholesale, Storage, Retail and Consumer Installation Operations) Rules, GN. No. 150 of 2022.

Accordingly, the public is hereby informed that any engagement by the two companies in the supply of petroleum products after revocation and suspension of the mentioned licenses will be deemed illegal and subject to legal penalties.

The Authority reaffirms its commitment to ensuring a competitive environment and a secure supply of petroleum products in the country by maintaining a fair level playing field for all.

Issued by:

Director General

EWURA.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI



MAMLAKA YA UDHIBITI WA
HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA)



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**KUSITISHWA NA KUFUTWA KWA LESENI ZA REJAREJA ZA BIDHAA ZA
MAFUTA YA PETROLI**

Dodoma, 4 Machi 2026.

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) inataarifu umma kwamba imefuta leseni ya Rejareja ya Bidhaa za Mafuta ya Petroli Na. PRL-2018-269 iliyotolewa kwa kampuni inayotambulika kwa jina Iyan Energy Limited ya Dar es Salaam kwa ajili ya kuendesha biashara ya Rejareja ya Bidhaa za Mafuta ya Petroli kwenye Kiwanja Na. 26 na 27, Barabara ya Pangani, jijini Tanga, na imesitisha kwa muda wa miezi sita, leseni ya rejareja ya Bidhaa za Mafuta ya Petroli Na.PRL-2022-296 iliyotolewa kwa kampuni inayotambulika kwa jina Crescent Energy Tanzania Limited kwa ajili ya kuendesha biashara ya Rejareja ya Bidhaa za Mafuta ya Petroli kwenye Kiwanja Namba 5, Kitalu 'N', Enelo la Chamakweza, Wilaya ya Chalinze District Mkoa wa Pwani, kwa kukiuka Sheria na masharti ya leseni.

Maamuzi haya yamefanyika baada ya Mamlaka kujiridhisha kwamba kampuni tajwa zimekuwa zikijihusisha na biashara ya Uuzaji wa Bidhaa za Mafuta ya Petroli kwa jumla kinyume na Kifungu Na.131 cha Sheria ya Petroli Sura ya 392 na Kanuni ya 9 na 11 ya Kanuni za Mafuta (Biashara ya Jumla, Uhifadhi, Rejareja na Matumizi Binafsi) Tangazo la Serikali Na. 150/2022.

Kufuatia taarifa hii, umma unataarifiwa kwamba kujihusisha kwa namna yoyote ile na kampuni hizi kwenye biashara ya usambazaji wa Bidhaa za Mafuta ya Petroli itakuwa kinyume cha Sheria na hatua kali zitachukuliwa.

Mamlaka itaendeleza dhamira yake ya kuhakikisha kuwepo kwa mazingira ya ushindani na upatikanaji salama wa bidhaa za mafuta nchini, kwa kudumisha uwanja wa ushindani ulio sawa kwa wadau wote.

Imetolewa na:

Mkurugenzi Mkuu

EWURA.